BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Sita – Tarehe 14 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

92. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Imekuwa kawaida sana kwa waathirika wa maafa walio wengi katika Mkoa wa Mjini Magharibi kuhamishiwa na kuhifadhiwa katika Skuli ya Mwanakwerekwe C. Hatua hii inatekelezwa bila ya kujali uendelevu wa masomo ya wanafunzi wa skuli hiyo, jambo ambalo limekuwa likijirejea bila ya Serikali kutafuta eneo mbadala na bila ya kuwafidia wanafunzi wa skuli hiyo kwa muda walioupoteza wakati wakiwapisha waathirika.

Je, ni upi mtazamo wa Serikali kuhusu jambo hilo na upi mpango wa kudumu wa kuliepusha jambo hilo linaloathiri elimu ya watoto wa Skuli ya Mwanakwerekwe C.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

22. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na wizi wa miundombinu katika barabara za Mkoa wa Mjini Magharibi, hasa katika barabara ya Benjamin Mkapa kutoka Mtoni hadi "Redio One" kwa kuibiwa waya za umeme na kuiwacha barabara kiza wakati wa usiku. Kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu na eneo lililoathirika zaidi ni la Mtoni kidatu ambako kuna vikosi viwili vya ulinzi vya JWT na JKU pamoja na kituo cha kusambazia umeme.

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi juu ya kukabiliana na hujuma hizo.

(b) Kwa kuwa ni muda mrefu sasa umepita tangu kuibiwa kwa waya hizo, ni kwa nini taa hizo hazijatengenezwa hadi hivi leo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

25. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mashamba ya mpira ya Mfenesini na Kichwele mwaka 2021, Mhe. Rais alitoa agizo kwa mashamba hayo ya mpira kushughulikiwa na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji badala ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, ili kutafuta wawekezaji wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu na ujenzi wa viwanda na kuwapatia wananchi makaazi bora kwa lengo la kuongeza uzalishaji na ajira kwenye viwanda.

Kwa kuwa agizo hilo limetolewa zaidi ya mwaka mmoja sasa Je, ni hatua gani zilizokwisha kuchukuliwa katika utekelezaji wa agizo hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

136. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa muda mrefu umepita bila ya Serikali kufanya tathmini kwa wananchi walioingia kwa kujenga nyumba zao za kuishi katika maeneo ya Furaha, Mvumoni na Mfikiwa kwenye eneo la uwanja wa ndege Pemba. Na kwa kuwa wananchi hao tayari wameshaelezwa na kufahamu kuwa wanatakiwa walipwe na kuondoka katika maeneo hayo baada ya kufanywa tathmini ya kiwango halisi cha malipo yao. Na kwa kuwa wananchi hao wamezitegemea fedha hizo kwa ajili ya kuendeshea maisha yao. Na kwa kuwa kila siku thamani ya fedha inaongezeka, jambo linalopelekea kiwango cha fedha hizo kuongezeka na Serikali kuzidi kupata hasara kwa kutokulipa fedha hizo kwa wakati.

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini hiyo ili wananchi wa maeneo hayo wapate haki zao kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa pamoja na Serikali kutokuendelea kujibebesha mzingo huo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

94. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tunalipongeza Baraza hili la Wawakilishi kwa kutunga sheria zenye maslahi kwa Wazanzibari, ikiwa ni pamoja na sheria zinazohusiana na utalii, ambazo kwa kiasi kikubwa zinatoa fursa za ajira na maslahi mengine ya utalii kwa Wazanzibari. Hata hivyo, sheria hizo zimekuwa hazifuatwi au hazisimamiwi ipasavyo kwa visingizio vya kutokuwa na sifa kwa Wazanzibari kwa ujumla wake.

(a) Je, ni ipi hali ya sasa ya utekelezaji wa sheria zinazohusiana na utalii kwa maslahi ya Wazanzibari, hasa katika kuongeza ajira kwa vijana.

(b) Je, ni zipi juhudi za Serikali za kuhakikisha sheria hizo zinatekelezeka kwa maslahi zaidi ya Wazanzibari.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

72. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Tunaipongeza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kutoa mafunzo kwa Wajumbe na watendaji wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na suala zima la mafuta na gesi. Katika semina hiyo wataalamu waliwaeleza washiriki kwamba masharti (*Fiscal Terms*) ya mkataba uliosainiwa kwa kitalu cha Zanzibar sio rafiki kwa wawekezaji, hivyo waliishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kurekebisha masharti hayo. Hata hivyo, kumekuwa na ukimya mkubwa kuhusu suala hili.

(a) Je, Serikali ina msimamo gani juu ya maoni ya wataalamu hao.

(b) Je, ni kitu gani kilichokwamisha utekelezaji wa mkataba huo na marekebisho yake.

(c) Kwa vile Disemba 2022 ndio mwisho wa mkataba huo, Je Serikali imejipanga vipi kumtafuta mkandarasi mwengine kwa kitalu ambacho kitarejeshwa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

4. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

   Katika kuimarisha afya za wananchi wetu, Serikali yetu inafanya juhudi kubwa za kuwahamasisha na kuwasisitiza wananchi wake juu ya suala zima la kuimarisha lishe bora kwa manufaa ya maisha yao. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo, inaonekana wazi kuwa kuna tatizo la uelewa na ufahamu mdogo wa wananchi walio wengi juu ya umuhimu wa chakula na lishe bora kwa wananchi hao.

   Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu juu ya chakula na lishe kwa wananchi wake wakiwemo watoto.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto :**

122. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

   Sheria ya Mtoto No. 6/2011 ni muhimu sana katika kulinda haki za watoto kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa kulinda haki za watoto (CRC- 1979). Hata hivyo, kutokana na kukithiri kwa vitendo vingi vya uvunjifu wa haki za watoto, imeonekana kuna mapungufu katika eneo la utekelezaji wa haki za watoto Zanzibar.

   (a) Je, Wizara imefanya tathmini yoyote ya kina kubainisha mapungufu hayo ya Sheria.

   (b) Je, ni lini Serikali wataileta Barazani Sheria hiyo kwa ajili ya kuifanyia marekebisho.

   (c) Je, Sheria hiyo ya Mtoto inazo Kanuni zake na kama haina zitatungwa lini.

**Wizara ya Afya:**

17. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

   Katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, kuna hospitali nyingi zilizojengwa tokea kipindi cha ukoloni ambazo mazingira yake kwa sasa hayako rafiki kwa kutolea huduma kwa wananchi wetu ikiwa ni pamoja na hospitali ya Vitongoji (Changuo).

(a) Je, ni lini Wizara itaifanyia matengenezo hospitali hii ya Vitongoji (Changuo) ambayo inaonekana kuwa katika hali mbaya kwa kukosa hata milango na vitasa ambavyo husaidia sana katika kutunza usiri na usalama wa wagonjwa wetu hospitalini hapo.

(b) Je, ni utaratibu upi unaotumika katika kuzifanyia matengenezo hospitali hizi za zamani ili kuzinusuru na kuweka usalama wa wagonjwa wanaofika kupatiwa huduma vituoni hapo.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

33. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Makongeni msingi ilijengwa madarasa matatu kupitia mfuko wa Mheshimiwa Mbunge pamoja na nguvu za wananchi. Kwa kuwa madarasa hayo yalikwishaezekwa.

Je, ni kiasi gani cha fedha za IMF (UVIKO – 19) kilichotumika kukamilisha mabanda hayo.

## IV. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**</u>

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

<u>**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**</u>

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**14 Septemba, 2022.** **<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**